## Waziri Mkuu azindua NBC Kidigitali



>UK3

Kisima Cha Maarifa

# FIKRA PEVU

fikrapevu | @fikrapevu | @fikrapevu

Tovuti: www.fikrapevu.co.tz | ISSN 3456-18 Toleo Na 37 Fikra Pevu Jumanne Machi 4, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100

# Marufuku kuswali swala ya Tarawehe




>UK 2

**Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari yapewa meno**

MICHEZO>>

## Arajiga, Kayoko waanza mafunzo ya VAR

Na Mwandishi Wetu

WAAMUZI 20 wakiwamo maarufu kama Ahmed Arajiga, Herry Sasii, Ramadhani Kayoko na Tatu Malogo, wameanza mafunzo maalum ya teknolojia ya usaidizi kwa waamuzi (VAR). Kozi hiyo yenye lengo la kuboresha ufanisi wa waamuzi hao inafanyika....

>UK 16



## ‘No Reform No Election’ propaganda iliyojaa upotoshaji wa Chadema

>UK3

**MAKALA NDANI**

- Tanzania haitakuwa salama, endapo DRC itaangukia mikononi mwa M23
- Tuyaenzi maridhiano kwa maslahi mapana ya Zanzibar

# Marufuku kuswali swala ya Tarawehe

Na Mwandishi Wetu

BARAZA Kuu la Waislamu katika Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC)limetoa amri ya kusitishwa kwa swala ya Tarawehe kuswaliwa misikitini katika miji ya Mashariki mwa nchi hiyo kutokana na sababu za kiusalama.

Miji iliyokumbwa na marufuku ya kuswaliwa swala hiyo ni Goma, Bukavu, Uvira na Baraka ambayo hali ya usalama hairuhusu waislamu kutoka usiku kwenda msikitini kwenda kufanya ibada hiyo.

Tukio la kusitishwa kwa swala ya Tarawehe liliwahi kutokea mwanzoni mwa miaka 90 wakati wa vita vya ghuba kule nchini Iraq ambapo serikali ya nchi hiyo chini ya hayati Rais, Sadam Hussein ililazimika kuchukua uamuzi huo mgumu kwa sababu za kiusalama.

Swala ya Tarawehe ni miongoni mwa sunna ambazo huswaliwa katika mwezi wa Ramadhan tu baada ya swala ya Isha. Kwa mujibu Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa akisisitiza swala ya usiku katika mwezi wa kufunga (Ramadhani), bila ya kuifaradhisha kwao.

Alikuwa akisema: Atakaye swali katika usiku wa mwezi wa kufunga, akiwa na imani na akitaraji malipo (kutoka kwa Allah (s.w),dhambi zake zilizotangulia husamehewa. (Muslim).

Marufuku ya Baraza hilo imetokana na hali ya usalama kuwa tete katika miji ya mashariki mwa nchi hiyo kutokana na vita inayoendelea kati ya majeshi ya serikali ya Congo DRC na waasi wa M23 ambao kwa sasa wanashikilia eneo kubwa la mashariki.

Taarifa ya Baraza hilo imeeleza hali ya usalama hairuhusu kutoka nje nyakati za usiku hivyo limewataka waislamu wote maeneo hayo kuchanganya swala ya Magharibi na Swala ya Isha na kurejea majumbani kabla ya giza kuingia.

Wakati hali ikiwa hivyo juhudi za kumaliza vita inayoendelea nchini zinaonekana kukatishwa tamaa baada serikali ya ya nchi hiyo kukataa kufanya mazungumzo ya maridhiano na waasi wa kundi la M23 ambalo limeteka maeneo makubwa mashariki mwa nchi katika miezi ya hivi karibuni.

Wiki iliyopita, serikali ya Uingereza ilitoa wito wa kuhusisha kundi la M23 katika "mazungumzo ya kujumuisha" kama sehemu ya juhudi za kupata suluhu ya kisiasa kwa mzozo huo.

Hata hivyo, katika mahojiano na BBC, Waziri Mkuu wa DR Congo, Judith Suminwa Tuluka, alisisitiza kuwa serikali yake inapendelea kuzungumza na Rwanda, nchi jirani ambayo inashutumiwa kwa kuunga mkono M23.

Kwa mujibu wa mamlaka za Congo, zaidi ya watu 8,500 wamepoteza maisha tangu mapigano yalipoongezeka mwanzoni mwa mwaka huu.Mamia ya maelfu wamelazimishwa kuondoka makwao wakihofia usalama wao wakati wa vita, ambapo wataalam wa Umoja wa Mataifa na wengine wakiangazia Rwanda kama nchi inayopiga jeki vita hivi.

'' Cha muhimu ni kwamba anayeleta vurugu na kutishia uhuru wa DRC ni Rwanda,'' Suminwa Tuluka anasema akinukuu ripoti kutoka kwa wataalam wa Umoja wa Mataifa mwaka jana ambayo ilitaja vikosi kati ya 3,000 na 4,000 vya Rwanda vilivuka kutoka mpaka wa Congo na vilisaidia wanamgambo wa M23.

Mazungumzo ya amani yaliyokuwa yakiongozwa na Angola mwaka jana mwezi Disemba yaligonga mwamba baada ya Rwanda kutaka serikali ya Congo izungumze moja kwa moja na waasi wa M23.

Waasi hao baadaye walionekana kuzidisha nguvu na kuteka baadhi ya miji mkuu kama vile Goma na Bukavu mwezi Januari na Februari.

Katika juhudi za pamoja za kutafuta suluhu zilizoanzishwa na mataifa ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, viongozi wake walitoa wito wa kusitisha mapigano, na kuondoka kwa '' vikosi vya kijeshi vya kigeni ambavyo havikualikwa'' kutoka Congo na pia kutaka pande zote mbili kukaa pamoja kusuluhisha.. wakijumuisha M23''.

## Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari yapewa meno

Na Mwandishi Wetu,

BODI ya Ithibati ya Waandishi wa Habari, (Journalists Accreditation Board-JAB) imetakiwa kuhakikisha kuwa, waandishi wa habari wote nchini wanazingatia sheria, kanuni, viwango vya juu vya weledi, maadili, uwajibikaji, na miongozo inayosimamia taaluma ya uandishi wa habari.

Maelekezo hayo ni kati ya maagizo saba yaliyotolewa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (MB), katika hotuba yake ya uzinduzi wa bodi hiyo uliofanyika tqrehe 03 Machi, 2025, katika Ukumbi wa Hotel ya Johari Rotana, jijini Dar es Salaam.

Profesa Kabudi amesema, Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari itasaidia kudhibiti uandishi usio wa kimaadili na kuongeza heshima ya taaluma hiyo, hivyo inatakiwa kuanza kwa kuwalea na kuwapa miongozo mbalimbali kuhusu taaluma yao.

Profesa Kabudi ameitaka pia Bodi hiyo kuhakikisha kuwa waandishi wa habari wanazingatia maadili ya taaluma kwa kutoa miongozo ya mafunzo ya mara kwa mara, na kuwa na utaratibu wa kushughulikia malalamiko na ukiukwaji wamaadili kwa haki na uwazi.

Agizo la pili kwa Bodi ni kuandaa na kusimamia utaratibu wa usajili wa waandishi wa habari kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma, huku akisisitiza kuwa mfumo huo unatakiwa kua shirikishi na wenye kuendana na maendeleo ya teknolojia na mazingira ya sasa ya sekta ya habari.

Ameitaka JAB kuhakikisha inashirikiana na vyombo vya habari, vyuo vya mafunzo ya uandishi wa habari, na wadau wengine ili kuhakikisha waandishi wa habari wanapata mafunzo ya mara kwa mara na kuwa na ujuzi wa kisasa.

Profesa Kabudi ameiagiza Bodi kuandaa programu za uelimishaji ili kuongeza uelewa wa umma kuhusu umuhimu wa taaluma ya uandishi kusimamiwa ipasavyo.

Amesisitiza kuwa ni muhimu Bodi pia ikasaidia kuhakikisha kuwa waandishi wa habari wanatumia teknolojia kwa manufaa ya taaluma yao bila kuvunja maadili, katika ulimwengu wa sasa wa kidijitali, ikiwemo kudhibiti matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii katika utoaji wa habari.

Kwa mujibu wa Profesa Kabudi Bodi inapaswa kushirikiana na mamlaka husika kuhakikisha kuwa waandishi wa habari wanafanya kazi zao kwa usalama bila vitisho, unyanyasaji, au vikwazo visivyo vya lazima, kwani Usalama wa wanahabari ni msingi wa uhuru wa vyombo vya habari.

Akitangaza kuzinduliwa rasmi kwa Bodi hiyo, Profesa Kabudi amesema, Serikali inatambua umuhimu wake, katika kuimarisha weledi, maadili, na uwajibikaji wa taaluma ya uandishi wa habari nchini, na kuahidi kuwa itaendelea kushirikiana nayo ili kuhakikisha taaluma ya habari inaimarika kwa manufaa ya taifa.

## Wizara ya madini,China wafanya majadiliano ya utafiti

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Madini Dkt. Steven Kiruswa amekutana na Balozi wa Jamhuri ya Watu wa China nchini Chen Mingjian katika kikao kilicholenga kujadili fursa na maeneo mbalimbali ya ushirikiano katika Sekta ya Madini ikiwa ni mwendelezo wa mazungumzo kati ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango na kiongozi huyo .

Katika mazungumzo yao, Dkt. Mpango aliiomba Serikali ya China kupitia balozi huyo kusaidia shughuli za utafiti wa madini Tanzania, ambapo baada ya mazungumzo yao, Serikali ya China imetuma wataalam wawili kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti ya nchini humo ili kufuatilia na kujua mahitaji ya utafiti na maeneo mengine ya mashirikiano kati ya Tanzania na China

''Kikao nilichokiongoza Machi 3 mwaka huu kimejadili maeneo ya ushirikiano, na sisi kwa upande wetu tumeweza kubaini maeneo matatu muhimu ambayo Serikali ya china inaweza kutusaidia katika shughuli za utafiti na kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara kulingana na mahitaji,'' amesema Dkt. Kiruswa.

Maeneo matatu ambayo wataalam wa Wizara wakiongozwa na Dkt. Kiruswa waliyoweza kuyabaini ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia (high resolution airborne geophysical survey) hususani kwa kuanzia eneo la Mkoa wa Dodoma;

Maeneo mengine ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa fursa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalam wa ndani katika maeneo ya teknolojia za kisasa kama vile ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za jiosayansi; na kusaidia kuleta teknolojia za kisasa za utafiti na uchakataji wa taarifa za utafiti wa madini ikiwa ni pamoja na matumizi ya ndege nyuki katika utafiti wa madini nchini.

Wengine walioshiriki kikao hicho ni pamoja na Kamishna wa Madini Dkt. Abdulrahman Mwanga Kamishna, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Jilojia na Utafiti wa Madini Tanzania, (GST) Dkt. Mussa Budeba, Mkurugenzi wa Huduma za Jiolojia (GST) Dkt. Ronald Massawe, Afisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Bw. Makamba, Makamba na maafisa kutoka ubalozi wa China nchini Bw. Chu Kun na wataalm kutoka Taasisi ya Jiolojia China Bw. Ren Junping na Bw. Sun Kai.



## Makonda awaonya wanaopandisha bei mwezi wa Ramadhani

Na Mwandishi Wetu

MKUU wa Mkoa wa Arusha,Paul Christian Makonda ameonya wafanyabiashara wa Mkoa wa Arusha kujiepusha na upandishaji wa gharama za vyakula vinavyotumika zaidi wakati huu wa msimu wa mfungo wa Mwezi mtukufu wa Ramadhan, akitangaza kuja na Operesheni maalum ya kutembelea maduka ili kubaini wafanyabiashara wanaotumia mfungo wa Ramadhan kujitafutia faida ya ziada.

"Niwasihi, mwezi huu ( Mwezi mtukufu wa Ramadhan) sio mwezi wa kutengeneza faida, mwezi huu ni wa kutafuta baraka, faida unayoitafuta inaweza kuna kukugharimu sana, ukajikuta umepata magonjwa yakala mpaka na mtaji wako. Wenzako wanapofunga kwaajili ya kumuomba Mwenyenzi Mungu, jitahidi na wewe uwe sehemu ya baraka ya kuhakikisha kuwa huwapi vikwazo." alisema Makonda.

Makonda pia kando ya kuarifu kuwa Mkoa unaandaa futari kwa ajili ya wananchi wa Mkoa wa Arusha, amewatakia Kheri pia Waislamu wa Mkoa wa Arusha kwenye mfungo waliouanza mwishoni mwa Juma lililopita sambamba na kwa Wakristo ambao wanatarajiwa kuanza mfungo wa Kwaresma hivi karibuni, akiomba kuwa funga zao zikafanyike kuwa baraka na kichocheo cha amani na Upendo katika Mkoa wa Arusha.

# Waziri Mkuu azindua NBC Kidigitali

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amesema kuwa huduma jumuishi za kifedha ni kiungo muhimu cha ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini na kuchochea maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Majaliwa ameyasema hayo jana alipozindua huduma mpya za kidijitali za Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) katika ukumbi wa Super Dome, Masaki jijini Dar es Salaam.Alisema Serikali kwa kutambua hilo imedhamiria kuendelea kushirikiana na wadau wote ili kuhakikisha sekta ya kifedha inazidi kuwa jumuishi, fanisi, na yenye tija kwa maendeleo ya Taifa.

Aliongeza kuwa katika vipindi tofauti, Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza mikakati ya Taifa ya kuboresha huduma jumuishi za kifedha."Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa 2023 – 2028 ni mwendelezo wa mafanikio yaliyopatikana kupitia Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha uliokamilika Desemba 2022"

Kadhalika,Majaliwa alisema,- jitihada nyingine ni kuandaa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa miaka 10 kuanzia mwaka 2024 hadi 2034. "Mkakati huu umeainisha malengo mahsusi ambayo kama nchi tunaazimia kuyatekeleza ili kufikia uchumi wa kidijitali."

Kwa upande wake, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Sauda Msemo amesema sekta ya fedha imeendelea kuwa na ustahimilivu na hivyo kuwezesha shughuli mbalimbali za kiuchumi kufanyika.

Aidha, Naibu Gavana huyo ametoa wito kwa taasisi zote za kifedha zifuate viwango bora vya usalama wa mitandao na kugundua haraka pale panapotokea udanganyifu wa aina yoyote.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi alisema lengo la uzinduzi wa huduma hizo za NBC kidijitali ni kuboresha utoaji wa huduma za kifedha na kuzifanya zipatikane kwa urahisi. "Huduma hizo ni pamoja na ufunguaji wa akaunti, kuhamisha fedha, kupata mikopo bila ya kwenda katika tawi."

Pia, Kiongozi huyo alitumia fursa hiyo kuishukuru Serikali kwa kuhakikisha wananchi wengi wana namba za NIDA ambazo zinarahisisha ufanyaji wa biashara, utambuzi wa mtu

## Jeshi la Zimamoto lachunguza moto maghala ya Ushirika

Na Mwandishi Wetu

JESHI la Zimamoto na Uokoaji mkoani Morogoro linaendelea kuchunguza chanzo cha moto ulioteketeza maghala ya Chama cha Ushirika wa Wakulima Morogoro (Mofacu), yanayotumiwa na Kampuni ya LMAX Limited kuhifadhi na kuchakata katani.

Moto huo ulizuka usiku wa kuamkia jana saa 6 usiku, karibu na kituo cha reli ya Kati katika Manispaa ya Morogoro.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Morogoro, Mkaguzi Ramadhani Khalid, akizungumza leo Jumatatu Machi 3, 2025, amethibitisha tukio hilo na kusema juhudi za kudhibiti moto zilifanikiwa kwa kiasi kikubwa, huku uchunguzi wa chanzo cha moto ukiendelea.

"Tumefanikiwa kudhibiti moto na kuokoa maghala matatu pamoja na ofisi za kampuni hiyo. Hata hivyo, uchunguzi wa kina utafanyika ili kubaini chanzo cha moto huu," amesema Khalid.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Kampuni ya LMAX Limited, Evidius Rwegasira, moto huo umeharibu shehena kubwa ya katani pamoja na mitambo ya uchakataji, na kusababisha hasara inayokadiriwa kufikia zaidi ya Sh700 milioni.

# Chadema yavuna milioni 64 kampeni ya 'Tonetone'

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Amani Golugwa, ametangaza kuwa kupitia kampeni ya Tone Tone, Watanzania wamechangia jumla ya Shilingi 64,315,150 tangu kampeni hiyo ilipozinduliwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika Makao Makuu ya CHADEMA, Mikocheni, Dar es Salaam, Golugwa amewashukuru Watanzania kwa imani yao na kujitokeza kwa wingi kuchangia chama kupitia njia mbalimbali.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hadi kufikia Machi Mosi mwaka huu, fedha zilizokusanywa kupitia akaunti ya NMB zilifikia Shilingi 16,858,461, huku michango kupitia namba ya M-PESA (0744446969) ikifikia Shilingi 3,997,109. Pia, kupitia mfumo wa Kulipa Bili kwa M-PESA, chama kimepokea Shilingi 5,785,670, wakati njia ya Mix Bill kupitia mtandao wa Mix by Yas imekusanya Shilingi milioni 1.7.

Licha ya mafanikio haya, Golugwa ameeleza kuwa kumekuwa na changamoto katika baadhi ya mifumo ya kuchangia, hasa kwenye namba ya M-PESA, ambapo baadhi ya wachangiaji walipata ugumu kufanya malipo. Hata hivyo, amebainisha kuwa tayari chama kimewasiliana na mamlaka husika ili kurekebisha hitilafu hizo na mfumo unafanya kazi kwa ufanisi.

"Nikiri kwamba zilitokea changamoto kadhaa katika mfumo wetu hasa kwenye namba hii ya 0744446969 na tumefanya mawasiliano na mamlaka husika na tupo katika kutatua changamoto hizo. Wachangiaji wengi wa Tone Tone walipata changamoto", ameeleza.

Kwa mujibu wa Golugwa, takwimu zinaonesha kuwa kuna kiwango kikubwa cha fedha ambacho kingeweza kuzidi Shilingi milioni 150 hadi 200, lakini mifumo ya malipo ilikuwa inawazuia baadhi ya wachangiaji. Amewahimiza Watanzania kuendelea kushiriki katika kampeni ya kuhakikisha wanadondosha matone matone ili kufanikisha dhamira ya chama.

Katika jitihada za kurahisisha michango, Golugwa ametangaza kuwa sasa Watanzania wanaweza kuchangia kupitia programu tumizi ya Sim Banking ya CRDB kwa mfumo wa malipo ya kujirudia (subscription payments). Pia, M-PESA ya Vodacom imeruhusu malipo ya kujirudia kwa walio na akaunti zao. Hata hivyo, kwa mitandao mingine, bado mfumo huo haujawekwa.

# Fahamu kuhusu maumivu ya Joints na mgongo

JOINTS/MAUNGIO

Ni sehemu ya mwili inayounganisha mfupa mmoja na mwingine,eneo kati ya mfupa na mfupa mfano goti,kiuno.Kumekuwa na changamoto nyingi sana inayohusu mfumo huu wa mifupa,joint pamoja na misuli ya mwili wako.

Na tatizo hili liko kwa watu wa jinsia zote.Kadiri ya umri unavyozidi kwenda ndivyo watu wengi huzidi kupata udhaifu katika viungo hivi,hususani kina mama lakini pia hata wana michezo,hufanyaji mazoezi mara kwa mara pia hupelekea kuisha na kuchakaaa ute ute au ulainishi katika joint kumalizika,

na hivyo kupelekea msuguano katika joints.

Matatizo ya mifupa.

Wako watu wengi sana hulalamika maumivu ya mgongo pasipo kujua chanzo hasa ni kipi,lakini kinachopata maumivu hapa ni mifupa pamoja na misuli na hii ni kwasababu ya ukosefu wa madini muhimu ambayo husapoti afya hii ya mifupa na misuli.

CHANGAMOTO ZITOKANAZO NA JOINTS/MIFUPA:-

- Mgongo kuuma sana
- Joints kuisha ute ute na maumivu makali
- Miguu kufa ganzi
- Misuli ya sehemu husika kukaza na kuuma
- Kushindwa kutembea kwa kawaida mpaka sapoti
- Magoti kupiga kelele kama unavunja muwa
- Magoti kuvimba.

HIKI NI CHANZO CHA MAUMIVU YA JOINTS NA MFUPA:-

1. Uzito mkubwa
2. Ukosefu wa ute ute kwenye viungo
3. Upungufu wa madini muhimu mwilini kama calcium
4. Kina mama waliofikia/kukaribia meno pouse(kukoma hedhi)
5. Ufanyaji mazoezi wa mara kwa mara bilakuzingatia lishe ya vilainishi kwenye viungo.

Tiba ya matatizo haya yanategemeana hasa kisababishi ni nini.

0715994721 Dr Musa Lucas

**kinachopata maumivu hapa ni mifupa pamoja na misuli na hii ni kwasababu ya ukosefu wa madini muhimu ambayo husapoti afya hii ya mifupa na misuli.**





# Tanzania haitakuwa salama, endapo DRC itaangukia mikononi mwa M23



Na Mwandishi Wetu

HAMNA wakati mwingine ambao Tanzania inahitaji DRC iliyotulia kama ilivyo Sasa.Rwanda ni ka Nchi kadogo sana, Ambako kana maeneo machache ya kimkakati linapokuja suala la uchumi , wako limited katika Resources .

Ndio Sababu Rais Paul Kagame Palipo na Migogoro anajitahidi kujiingiza na kusaini mikataba ya kudumu. Ni nani anajua hapo Msumbiji Rwanda atakaa miaka mingapi?.Embu ifikirie Rwanda yenye ushawishi na base za kijeshi na silaha nzito nchini Msumbiji, Uganda, DRC, Rwanda , Burundi , Tutatoboa?

Kagame kwa Rwanda, anazuga tu Kupambana na FDLR ,ila lengo ni Utajiri wa DRC, Dhahabu , Cobalt, Tantalam, Tin , Coltan , madini muhimu sana katika Teknolojia za kisasa hapa Duniani.

Kwa Kujua Udhaifu Mkubwa wa Jeshi la Kongo ambalo limezidi kuangamiziwa Kwa Rushwa, Ukosefu wa mishahara , Uwekezaji Mdogo wa Jeshi , M23 hawatoweza kuishia mashariki ya DRC , Ngoma itaenda tu mpaka Kinshasa , Ndoto ya Kagame ni kutumia Minority Kuitawala DRC na akifanikiwa hili basi Tanzania matatizo yataanza.

Tanzania kupitia JWTZ ni lazima ihakikishe Rwanda haipati nafasi ya kukaa mashariki ya DRC na hata kuikali DRC kwa ujumla.

KIUCHUMI,ni lazima Kumfanya Rwanda aendelee kua Mtegemezi wetu , Kuruhusu Rwanda ikae DRC maana yake ni kuruhusu Biashara ya Madini Kati ya Ulaya/Marekani na Rwanda , naongezeko lolote la Biashara ya Madini Kwa uwazi Kati ya Mataifa hayo na Rwanda, maana yake kunaenda kufungua Fursa nyingi sana Nchini Rwanda, na Ni hizo Fursa ndizo zinazoenda kufubaza Maendeleo ya Nchi yetu.

KIUSALAMA, Rwanda Ndani ya DRC kama ambavyo amekua na Tamaa na lugha mbaya juu ya Taifa letu, maana yake ni kua ataendeleza Chokochoko tu ambazo tutahitajika Kupambana na Rwanda katika 3 fronts Kusini kutokea Msumbiji, DRC Rwanda, sahizi ana Ndugu yake Uganda , Burundi ndo kabisa !, Kagame hashindwi kuanziasha Vikundi vya waasi .

JWTZ ni lazima wahakikishe wanampiga m23 na kumuondoa kabisa mashariki ya DRC, wasiruhusu Rwanda watumie utajiri wa DRC kujiimarisha kijeshi na kuimarisha uwezo wao wa kijeshi ndani ya drc, utajiri wa DRC-mikononi mwa rwanda maana yake ni kuruhusu rwanda kujitanua na kutengeneza vikundi vya waasi wenye uwezo mkubwa wa kijeshi ,endapo Rwanda atalifanikisha hilo, basi tanzania tutakua tumepoteza uhuru wetu tulionao kijeshi kwa afrika mashariki nzima.

Ukijiuliza kwanini Israel anapambana sana kuhakikisha mashariki ya Kati hamna mwenye Nguvu zaidi yake kijeshi, basi utakubali kua Kwa ajili ya manufaa ya muda mrefu, hamna Taifa zaidi ya Tanzania linalotakiwa kua na Nguvu .

Kagame apigwe, na azuiwe, ikiwezekana apelekewe vita nchini kwake, Rwanda ni ndogo sana, uchumi wake ukivurugwa ,itamchukua miaka na miaka kujijenga upya, tofauti na sisi Tanzania tulio na taifa kubwa na lenye utajiri mwingi.

**Tanzania kupitia JWTZ ni lazima ihakikishe Rwanda haipati nafasi ya kukaa mashariki ya DRC na hata kuikali DRC kwa ujumla.**




# Mbowe shikilia hapohapo mpaka waje kuomba po!

Na Yahaya Msangi

MLIMFUKUZA tajiri hamkujua mto utakauka?Nani aliawashauri muanze kutukana mamba kabla hamjavuka mto. Hvi wakati mnatoa kashfa na maneno ya kejeli kwake hamkujua kwamba mwamba ni bonge la jitu ndani ya Chadema.

Mwenyekiti Mstaafu Freeman Mbowe bana kimya hivyohivyo tuone kama matone yatatengeneza mto.Wenye maono ya mbali tuliwaonya mapema lakini hamkutaka kusikia.Mkakaza mafuzu kana kwamba yale tuliyowaonya hayawahusu.

Kwa sasa Chadema iko ICU kiuchumi.Mwamba Mbowe ameondoka na mirija yote ya kuleta fedha ndani ya chama. Wakati wa kampeni za uchaguzi mlinukuliwa kwa nyakati tofauti mkisisitiza kwamba mmejipanga kuipeleka chadema nchi ya ahadi.

Really tambo zote zile kuwa mnakuja na jambo kubwa ni hili la kuomba matone?Hivi kwani hii ni mara ya kwanza nyie kuomba hela zichangwe kimtandao? Kama huko nyuma ilibuma matone ndio itaweza?Kama mpaka sasa hamjagundua uongozi mpya hauna jipya basi jiandaeni kwa kilio kikubwa oktoba.

Matone? Ni chanjo ya surua au pepopunda?

Mtaweza kusimamisha wagombea majimbo yote kama Mbowe? Kwa matone?Ni mwezi na kiduchuu mumechaguliwa. Hamna Cha maana zaidi ya kwenda kupokelwa Ikungi Tarime, kusema Wassira Mzee, maaskofu wamehongwa mabilioni, kupayuka no reforms no election huku mkijua uchaguzi upo, n.k.

Ujinga Fulu!

Mlimtuhumu Mbowe kapoteza uwezo wa kuitisha serikali, akiitisha maandamano anaenda na mwanae. Haya nyie itisheni maandamano. tuone? Zuieni uchaguzi tuone? Kataeni kuongea na serikali tuone?

**Mwenyekiti Mstaafu Freeman Mbowe bana kimya hivyohivyo tuone kama matone yatatengeneza mto. Wenye maono ya mbali tuliwaonya mapema lakini hamkutaka kusikia.Mkakaza mafuzu kana kwamba yale tuliyowaonya hayawahu**



# Tuyaenzi maridhiano kwa maslahi mapana ya Zanzibar

Na Sarah Mossi

Takriban wiki kadhaa sasa tumeshuhudia na kusikia matamko mbalimbali kutoka kwa viongozi wa chama kikuu cha upinzani Zanzibar ACT- Wazalendo wakitishia kujitoa kwenye Serikali ya Umoja wa KItaifa iliyoasisiwa na Rais Mstaafu Amaan Abeid Karume na aliyekuwa Mwenyekiti wa CUF wakati huo Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad.

Kauli hizi kwa kiasi fulani zimeleta sintofahamu kubwa kwa wananchi ambao ndio wadau wakubwa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa maana wao ndiio waliopiga kura ya maoni kukubali kuwapo kwa serikali hiyo visiwani hapa.

Ikumbukwe kuwa Serikali ya Umoja wa kitaifa haikuja kwa kubahatisha, Serikali hiyo iliundwa baada ya vyama viwili vilivyoshabihiana kwa karibu sana katika matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa 2000 kukubaliana na hatimaye kutaka maoni ya wapiga kura ambao ni wananchi namna gani wataweza kuendesha serikali na kuondoa ile sintofahamu iliyokuwapo miaka mingi baada nchi kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Haikuwa kazi rahisi kufikia makubaliano hayo kwa maana vyama vyote viwili vilikuwa vikivutia kwake na ilifikia mahali mojawapo ya chama kilitishia kujiondoa kwenye vikao vya kujadili Serikali ya Umoja wa kitaifa huku chama kingine kikitishia kukifufua chama cha Afro Shirazi Party (ASP), mradi tu wagawane mbao.

Lakini hatimaye walifikia makubaliano kwamba amani ya Wazanzibar ni kitu muhimu zaidi kuliko kitu choche na hivyo ukaanzishwa mchakato wa kura ya maoni ambayo hiyo ndio ikatoa mustakabali wa wapi tunaelekea.Serikali ya Umoja wa Kitaifa sio matakwa ya vyama, serikali hii imetokana na maoni ya Wazanzibar wenyewe.

Wazanzibar wenyewe ndio walichagua kuchoka na siasa za uhasama walichagua amani na utulivu ni bora zaidi kuliko chama chochote cha siasa au kuliko kitu chochote. Mabadiliko ya kumi ya Katiba ya Zanzibar yaliyoifanya Katiba ya Zanzibar kubadilika yote na kuundwa muundo mwingine wa utawala yaliifanya Zanzibar kutulia kwa kiasi fulani pamoja na kuwapo changamoto kadhaa.

Maridhiano ni jambo muhimu sana katika kuongoza nchi kama zipo changamoto katika kufikia yale makubaliano yaliyozaa serikali hii yanapaswa kushughulikiwa ili kuondoa malalamiko ya mara kwa mara.

Kikosi kazi kilichoundwa kuangalia changamoto mbalimbali katika mwenendo wa kisiasa nchini kinapaswa kuangalia tatizo liko wapi ndani ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ili nchi iweze kutulia.Wananchi wa Zanzibar wangependa kuingia kwenye uchaguzi mkuu ujao kwa amani huku wakihakikishiwa usalama wao.

Kama nilivyogusia hapo awli, Serikali hii ilipatikana kutokana na maoni ya kura za wananchi, hivyo wananchi wenyewe bado wanaitaka serikali hii kuendelea mbele. Na kuendelea mbele kwa Serikali hii inapaswa basi kuhakikisha yale makubaliano yafanyiwe kazi kama vile walivyokubaliana.








# No Reform No Election' propaganda iliyojaa uposhaji wa Chadema

Na Baraka Mussa,Kigoma

KATIKA siasa, kuna mbinu mbalimbali zinazotumiwa na vyama vya siasa hasa vya upinzani ili kushawishi umma kuelekea upande wao wa fikra(upande wao wa Kisiasa). Moja ya mbinu hizo ni propaganda za kupotosha ukweli ili kuunda taharuki na mgawanyiko wa kisiasa.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA),chini ya uongozi wa Mwenyekiti,Tundu Lissu, kimeanzisha ajenda inayoitwa "No Reform, No Election" (Bila Mabadiliko Hakuna Uchaguzi). Makala hii itachambua kwa kina ajenda hiyo, itaeleza jinsi ina malengo ya kupotosha wananchi, na na tutaelezea siri ya ajenda yao ya kupotosha ukweli.

1. Upotoshaji wa ukweli na ajenda yenye maslahi binafsi

CHADEMA imekuwa ikidai kuwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) haina uhuru na kwamba mfumo wa uchaguzi hauwezi kuhakikisha haki. Hata hivyo, hoja hizi hazina msingi na ni dhaifu kwa sababu zifuatazo:-

wa marekebisho ya sheria ulifanyika kwa maridhiano Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliongoza maridhiano ya kitaifa na mchakato wa mabadiliko ya sheria za uchaguzi uliopelekea kuanzishwa kwa Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Na. 2 ya 2024 iliyotangazwa kutumika 12 Aprili 2024.

Pamoja na mabadiliko ya kuitwa Tume huru ya Uchaguzi. Hii inathibitisha kuwa madai ya CHADEMA kuwa hakuna mabadiliko ni uongo wa wazi na Chadema wanajenda binafsi na sio ajenda yenye maslai ya Taifa.

Uhuru wa vyombo vya habari umeimarika Katika kipindi cha Rais Dkt. Samia, vyombo vya habari vinafanya kazi bila vikwazo, hata kuripoti upotoshaji unaofanywa na baadhi ya wanasiasa wa upinzani kama upotoshaji wao unaripotiwa.

Ikiwa kweli kungekuwa hakuna uhuru wa maoni, je, kwa nini propaganda zao na mikutano yao inaripotiwa waziwazi?,Chadema na lisu ni wakupuuza kabisa ni waongo na wanamalengo mabaya ya kupotosha ukweli kabisa,wananchi tunapaswa tuwapuuze maana hawana malengo mazuri na Taifa.hoja zao zimejaa ubinafsi na sio maslai ya Taifa.

Ruhusa ya mikutano ya siasa Serikali ya Rais Dkt.Samia imeondoa vikwazo vya mikutano ya hadhara ya kisiasa, kuruhusu vyama vya upinzani kufanya siasa zao kwa uhuru pamoja na kufanya maandamano ambayo yalikosa uungwaji Mkono.

Hii inaonyesha dhamira ya Rais Dkt. Samia ya kukuza demokrasia, kinyume na madai ya CHADEMA yaungo na yenye lengo la kupotosha ukweli.Rais Dkt.Samia anakubalika kimataifa kama rahisi bora na muumini wa haki na Demokrasia,Chadema hawana hoja bali wanapotosha ukweli .

2. Propaganda yao na namna wanavyojaribu kupotosha umma

Ajenda ya No Reform, No Election ni propaganda ya taharuki (Fear Appeal Propaganda) inayolenga kusababisha hofu kwa wananchi ili kupata huruma ya kisiasa hii tumeshawashtukia. Hii ni mbinu inayotumiwa na vyama vya siasa duniani kote vinavyokosa ushawishi wa sera.

Katika kitabu maarufu cha *"Propaganda, The Formation of Men's Attitudes"* cha Jacques Ellul, mwandishi anaeleza kuwa vyama vya siasa ambavyo vimeshindwa kushawishi wananchi kwa sera kama CHADEMA huanzisha propaganda za kutengeneza mgawanyiko na taharuki kwa lengo la kuchelewesha uchaguzi au kudhoofisha imani ya umma kwa taasisi za serikali.

Siri Iliyojificha ya Ajenda ya "No Reform, No Election"

CHADEMA wanajua kuwa hawajajipanga kushiriki uchaguzi wa 2025 na wanatambua kuwa hawana nafasi ya kushinda dhidi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho kimejikita katika maendeleo ya wananchi. Badala ya kujipanga kwa uchaguzi, wanatafuta sababu za kuhalalisha kushindwa kwao kabla hata ya uchaguzi kufanyika.

3. Wajibu wa CHADEMA Baada ya Uchaguzi wao wa ndani

Baada ya CHADEMA kufanya uchaguzi wake wa ndani, walipaswa kufanya yafuatayo kama chama makini cha siasa na sio upotoshaji.

Kujenga chama kutoka mashina,tawi hadi taifa Katika siasa imara, chama kinatakiwa kuwa na mtandao wenye nguvu wa wanachama na viongozi wake. Badala yake, CHADEMA hawana hata viongozi wa matawi na mashina katika maeneo mengi. Kisha wanaanza na ajenda binafsi yenye malengo ya kuleta taharuki ambayo wao wanajua kabisa ni kinyume cha sheria.

Kuandaa sera mbadala Vyama vya upinzani vinavyoheshimika ulimwenguni kama Labour Party ya Uingereza na SPD ya Ujerumani vinashinda uchaguzi kwa kuandaa sera bora, si kwa propaganda za vurugu kama zinavyo fanywa na Chadema ni wazi kabisa Lisu ni mwanaharakati mwenye malengo ya kuupotosha uma na kunidhania kuwa ajenda yao uchwara itaungwa mkono,Chadema ni wazi kabisa sio chama makini na jenda yao watashindwa mapema kabisa.

Kufanya siasa za kiungwana Siasa ni kushindania sera bora kwa hoja. Kuanzisha ajenda ya "hakuna uchaguzi" badala ya kujiandaa kushiriki uchaguzi ni dalili ya chama kisichojiamini na niwazi kabisa kinajua hakijajiandaa na tayari wanajua wameshashindwa wanatafuta kichaka cha kijifichia,Tunapaswa kuwaambia Chadema watanzania sio wajinga na mwaka huu watanzania hawadanganyiki na ajenda za chadema zenye malengo mabaya .

4. Udhaifu wa hoja za CHADEMA

(i) "Tume haina uhuru"

Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inasisitiza uhuru wa tume. Kifungu cha 8(1)kinahakikisha tume inafanya kazi kwa uhuru na hakuna mamlaka inayoweza kuingilia.

(ii) "Tume hii inasababisha watu wetu kupigwa na kuuawa"

Hakuna ushahidi wa kisheria au kitaalamu unaothibitisha madai haya. Madai haya ni mbinu ya kutafuta huruma ya kisiasa na kupotosha ukweli ,Chadema ni wazi kabisa sio chama Makini na hakina malengo mema na taifa letu,watanzania tunapaswa kukipuuza hiki chama.

(iii) "No Reform, No Election"

Kwa mujibu wa Ibara ya 77 ya Katiba yetu ya Tanzania, uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani lazima ufanyike kila baada ya miaka mitano. Hakuna kifungu kinachoruhusu kusogeza mbele uchaguzi kwa sababu ya matakwa ya chama kimoja kama wanavyodai chadema eti uchaguzi usogezwe mbele.ni wazi kabisa Chadema hawana hoja yenye malengo mazuri na hawana hoja yenye dhamira njema na Taifa letu.

(iv) "Tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha uchaguzi haupo"*

Kifungu cha *124 cha Kanuni za Uchaguzi kinaeleza kuwa yeyote anayepanga au kujaribu kuzuia uchaguzi kufanyika anaweza kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

5. Ushauri kwa Wananchi wenye mapenzi mema na Taifa

1.Kupuuza propaganda za taharuki

Wananchi wasidanganywe na vyama vinavyotafuta huruma badala ya kunadi sera kama Chadema ,hiki chama hakifai kabisa.

2. Kushiriki uchaguzi kwa wingi Kila Mtanzania ana wajibu wa kushiriki uchaguzi kama njia ya kidemokrasia ya kuamua viongozi. hivyo wananchi tunapaswa kujiandaa kushiriki uchaguzi mwaka 2025.

3. Kutambua kuwa uchaguzi hautasogezwa mbele.Kwa mujibu wa Katiba, uchaguzi utaendelea kama ulivyopangwa bila kujali ajenda za chama chochote cha siasa.Hivyo Chadema ni wakupuuza kabisa .

Ajenda ya No Reform, No Election ni propaganda ya kisiasa isiyo na msingi wa kisheria wala ukweli wa kisiasa. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameimarisha uhuru wa vyombo vya habari, amewaruhusu wanasiasa kufanya mikutano, na amefanikisha mabadiliko ya sheria kwa maridhiano. Ni wajibu wa Watanzania kuendelea kumuunga mkono Rais Dkt.Samia.

Wananchi wanapaswa kuwa makini na propaganda za taharuki zinazotumiwa na CHADEMA na badala yake waendelee kushiriki uchaguzi na kuchagua viongozi kwa misingi ya maendeleo na sera bora.

**Kwa maoni.**
**Baraka Mussa,Kigoma**
**Mjumbe halmshauri kuu ya CCM Kigoma Mjini.**
**barakamussa75@gmail.com.**

# Jinsi 4R za Rais Samia zinavyoweza kutatua mgogoro wa DRC

NINAPOTAFAKARI kwa kina mgogoro unaoendelea nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), ninakumbuka falsafa ya 4R ya Rais Samia Suluhu Hassan. Kama ingetekelezwa ipasavyo, inaonekana kuwa ingeweza kuumaliza mgogoro huu mara moja.

Swali linalojitokeza: Kwa nini wasaidizi wa Rais Samia hawachukui hatua kuhakikisha falsafa hii inatumika katika kutatua mgogoro huu?Kazi ya kiongozi ni kuonyesha njia, kisha wengine wafuate. Rais Samia alipoingia madarakani, alikuta nchi ikiwa na changamoto za kisiasa, na akaja na falsafa yake ya 4R kama suluhisho la kuzitatua. Mgogoro wa DRC unaohusisha waasi wa M23 pia ungeweza kushughulikiwa kupitia falsafa hii na kufikia suluhisho la haraka.

Falsafa ya 4R inajikita katika misingi ya: Maridhiano (Reconciliation), Ustahimilivu (Resilience), Mageuzi (Reforms) na Ujenzi wa Taifa upya (Rebuilding).Kinachoendelea DRC ni matokeo ya mgogoro wa muda mrefu. Serikali ya DRC inahesabu M23 kama waasi wa Kinyarwanda na inataka waondoke kwenye ardhi yake. Kwa upande mwingine, M23 wanajitambua kama Wanyamulenge, wakazi wa asili wa Goma, hivyo hawaoni sababu ya kuondoka. Rwanda inaunga mkono madai yao ili wapate haki yao ya kutambuliwa.

Fursa kwa Tanzania katika usuluhishi

Wiki iliyopita, nilimpongeza Rais Samia kwa kuitisha mkutano wa wakuu wa nchi za SADC na EAC kujadili mgogoro wa DRC. Hata hivyo, nilisikitika kuona kuwa taarifa za mkutano huo zilitolewa kwa Kiingereza, Kifaransa na Kireno pekee, bila Kiswahili. Tanzania, ambayo ni mwenyeji wa mkutano huo, inatumia Kiswahili, Goma ni eneo linalotumia Kiswahili, na hata waasi wa M23 wanazungumza Kiswahili. Kwa nini basi Kiswahili kimepuuzwa?

Pia, mkutano huo ulijadili mgogoro wa DRC bila kuwahusisha waasi wa M23, jambo ambalo ni makosa. Haiwezekani kupata suluhisho la mgogoro bila kuwashirikisha wahusika wakuu. Hatua ya kwanza katika usuluhishi ni maridhiano na kusitisha vita.

Mgogoro huu ni fursa adhimu kwa Tanzania kuonyesha uwezo wake wa kutatua migogoro ya Afrika kwa njia za Kiafrika. Ikiwa 4R zitatumika kwa ufanisi, Rais Samia ataonyesha kuwa Tanzania inaweza kuwa kinara wa suluhisho za Kiafrika kwa migogoro ya bara hili.

Njia ya kutatua mgogoro wa DRC kwa 4R ni pamoja na maridhiano (Reconciliation) Serikali ya DRC inapaswa kukubali kuwa M23 ni sehemu ya raia wake na kufanya mazungumzo ya maridhiano ili kusitisha vita. Lakini pia ustahimilivu (Resilience), yaani DRC inapaswa kujifunza kuvumilia na kukubali uwepo wa raia wake wenye asili ya Rwanda.

Vilevile, M23 wanapaswa kuonyesha ustahimilivu kwa kusitisha mapambano na kukubali mazungumzo. Njia nyingine nia mageuzi (Reforms), yaani M23 waachane na jina la waasi na badala yake waonekane kama jeshi la ukombozi wa Banyamulenge. Lazima kufanyike mageuzi ya kijeshi na kisha M23 waingizwe rasmi ndani ya jeshi la DRC.

Na mwisho ni ujenzi wa Taifa upya (Rebuilding), DRC inapaswa kujengwa upya kama taifa lenye mshikamano, linalowahusisha raia wake wote bila ubaguzi wa asili.

Ikiwa falsafa ya 4R itatumika ipasavyo, mgogoro huu unaweza kutatuliwa ndani ya muda mfupi. Suluhisho la kweli linatokana na ukweli kwamba M23 ni sehemu ya DRC na wanapaswa kushirikishwa katika ujenzi wa amani badala ya kuendelea na vita. Rwanda na Uganda zitaacha kuwaunga mkono M23 pindi DRC itakapokubali ukweli huu na kufanya maridhiano ya kweli.

Rais Samia ana nafasi ya pekee ya kulitatua hili kwa kutumia falsafa yake. Ikiwa hatua sahihi zitachukuliwa, Tanzania itang'ara kimataifa kama taifa linaloweza kutoa suluhisho kwa migogoro ya Afrika.

Nimemtwisha Rais Samia jukumu la kuutatua mgogoro huu, kwasababu mgogoro huu ni fursa adhimu kwa Tanzania na Rais Samia,Kiafrika,kikanda na kimataifa,kuiambia dunia matatizo ya Afrika,yanahitajisuluhisho la ki Afrika na Afrika,tuna viongozi wenye uwezo wa kuutatua mgogoro kia AfrikA.Pia kumalizika kwa mgogoro huu ni fursa ya kiuchumi kwa Tanzania kupitia Dar Port.Hili Mama analiweza na liko ndani ya uwezo wake. Mungu mbariki Rais Samia, Mungu ibariki Tanzania.






# Tuitunze amani yetu kwa wivu mkubwa kwani ndiyo Uhuru Wetu

Na Maliki Maliki,Chamwino,DODOMA

NELSON Mandela aliwahi kusema ''Fedha haziwezi kutuletea mafanikio,ila uhuru wa kuzitafuta ndiyo utakaotuletea maendeleo'' pia baba wa Taifa Mwl J.K Nyerere aliwahi kusema maneno ya fauatayo ''Maendeleo ya kweli ndiyo msingi wa amani ''

April 26 mwaka jana Rais wa Tanzania DR SAMIA SULUHU HASSANI akihutubia wananchi pamoja na viongozi mbalimbali wakati wa kilele cha sherehe za miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zilizofanyika katika uwanja wa uhuru Dar es salaam aliwataka watanzania katika kutekeleza Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioasisiwa mwaka 1964 watanzania hatuna budi kutekeleza kwa vitendo falsafa ya 4R.



Rais Samia ameutambulisha uongozi wake ndani ya ulimwengu wa falsafa yake ya R nne [4R] zikiwa na maana ya Maridhiano[Reconciliation ],Mabadiliko [Reforms],Ustahamilivu[Resilience] na Kujenga upya [Rebuilding.Rais wetu alilisitiza kuwa watanzania tukiziishi hizi falsafa za 4R hayo ndio yatakayo endelea kujenga amani na utulivu wa kudumu nchini kwetu na kuleta maendeleo endelevu .

Rais wetu mama Samia kwa nyakati tofauti ,amekua akisisitiza wasaidizi na watendaji wa serikali na viongozi wa chama cha mapinduzi [CCM] kusimamia 4R katika utekelezaji wa majukumu yao ,akisema ndiyo mwelekeo wa kujenga Taifa lenye umoja na mshikamano

Akiwa kwenye kumbukumbu ya miaka 63 ya uhuru wa Tanganyika Rais akatoa ujumbe kupitia mitandao ya kijamii akiwatakia heri watanzania na mnukuu'' Kheri ya Miaka 63 ya uhuru kwetu sote .Tutumie siku hii njema kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa hatua kubwa tunazoendelea kupiga kimaendeleo kama Taifa .

Tujivunie na kwa Pamoja tuendelee kufanya kazi ya kuzilinda na kuzitunza tunu za AMANI UMOJA na MSHIKAMANO ambazo ndizo nguzo za mafanikio yetu.Watanzania wenzangu sote tunajukumu la kuzilinda 4R katika Maisha yetu ya kila siku,kila mtanzania akiishi kwenye falsafa hizi za 4R utailinda amani,tukilinda amani tunapata nafasi ya kuendeleza nchi yetu kwa maendeleo.

Kukiwa na amani ,Watoto wetu watasoma kwa utulivu,wafanya biashara watafanya biashara, wagonjwa watapata matibabu kwa utulivu ,tutakua huru kutembea kokote kufanya shughuli za maendeleo waswahili wana msemo wao '' bora ugali dagaa kwenye amani kuliko wali nyama vitani'' kauli hii kila mtu atafakari

Watanzania wenzangu tuzitafakari pia nukuu ya Mzee Mandela aliyosema ukiwa huru ndio unakua huru kutafuta fedha [Maendeleo] na Baba wa Taifa kasema maendeleo ya kweli yapo kwenye amani

Kila mmoja amsisitize mtanzania mwenzake kuziishi 4R kila ukitaka kufanya jambo lolote wafikirie watanzania wenzako katika miaka 63 ya uhuru wetu ,je jambo lako unalofanya linailinda amani yetu ,ukiona alilindi amani liache.

> **Fedha haziwezi kutuletea mafanikio,ila uhuru wa kuzitafuta ndiyo utakaotuletea maendeleo**

# Athari zitokanazo na ulaji wa udongo kipindi cha ujauzito

MJUMUISHO wa tabia za ulaji wa vitu visivyo vyakula huitwa Pica, Hali hii inaweza kumpata mtu yeyote yule,lakini kwa upekee kabisa tujaribu kuona mojawapo ya aina za “Pica” inayotokea kwa wanawake wajawazito ambayo ni ulaji wa udongo. Hali hii hutoa maana ya kuashiria uwepo wa upungufu wa virutubisho muhimu pamoja na uchache wa madini ya chuma mwilini

Hali hii ya kuendelea kula udongo ikikithiri inaweza kusababisha kutokea kwa tatizo la choo kigumu,kuziba kwa utumbo,kuzaliana kwa minyoo kwenye tumbo na utumbo,kuvujia kwa damu tumboni pamoja na maumivu ya tumbo.

Udongo unaweza pia kuzuia ufyozwaji wa madini na virutubisho muhimu mwilini na inaweza pia kusababisha kupotea kwa hamu ya kula. Ikiwa mambo haya yatatokea,mtoto anaweza kukabiliwa na upungufu mkubwa wa virutubisho hivyo nakushindwa kukua vizuri tumboni kwa mama

MUHIMU kwa wanawake wote wajawazito wakijizuia kutumia udongo,pia ni muhimu kwao kufanya uchunguzi ikiwezekana pia kutilia maanani njia mbadala za kujipatia madini ya chuma badala ya kula udongo ili kujiepusha na matatizo yaliyoelezewa hapa. Hali hii (Pica) huweza kujitokeza kwa namna nyingi,wengine ikiwafanya wapende sana kula karatasi,barafu,sabuni,majivu,mkaa,magadi soda pamoja na nguo/matambara

Chukua tahadhari mapema

Imeandikwa na DK. Harun Mmari

Kama unahitaji ushauri wowote wakiafya wasiliana na Dk. Harun Mmari kwa nambari 0625940497

**Udongo unaweza pia kuzuia ufyozwaji wa madini na virutubisho muhimu mwilini na inaweza pia kusababisha kupotea kwa hamu ya kula. Ikiwa mambo haya yatatokea,mtoto anaweza kukabil**





# Si vibaya watoto wetu wakawa na majinamawili la kiasili na la Imani anayoamini

Na Zaituni Mnubi



BARAZA la Kiswahili Tanzania(BAKITA) limeombwa kutumia kanga iitwayo Kisutu kutumika kama alama ya Lugha ya Kiswahili nchini Tanzania na popote Duniani. Hili ni ombi kutoka kwa

Wakalimani wa Lugha ya Kiswahili wanaofanya kazi ya kutafsiri Kiswahili nje ya Tanzania.

Vazi la kanga ndio vazi rasmi la waswahili wa Tanzania, likitumika pia kama ubao wa kujifunza Lugha yetu pendwa ya Kiswahili kutokana na asili ya vazi hilo kubeba methali, misemo na maneno yenye mafunzo mbalimbali yanayokua yameandikwa.

Wakalimani wamekuja na wito ikiwa ni mikakati ya maandalizi ya kuelekea siku ya lugha ya Kiswahili Duniani ambayo hufanyika kila Julai 7 kwa mwaka na uwepo wa khanga hiyo iwe ni alama ya sherehe hiyo.

Kanga hiyo inayoitwa Kisutu ni mojawapo ya kanga kongwe iliyobuniwa na jamii ya waswahili ya Tanzania inayoeleza historia na mazingira halisi ya jamii ya mswahili wa Tanzania. Toleo la kanga ya Kisutu linakisiwa kuwepo na kuvaliwa na waswahili wa Tanzania kwa zaidi ya miaka 176.

Marembo ya kanga mara zote huakisi mazingira ya jamii ya waswahili mfano wa marembo mengi ya kanga ni minazi, embe, korosho, mpunga, nakadhalika ikiashiria mazingira halisi ya Mswahili wa Tanzania.

Kanga ya Kisutu au wengi hupenda kufupisha Sutu ni kanga yenye rangi ya wekundu wa damu ya Mzee na imepambwa kwa marembo ya moyo, madoa ya ndege kanga, marembo ya kipepeo, nakadhalika.

Neno Kisutu lilitokana na neno la Lugha ya kizaramo “Msutu” likimaanisha msitu ambao ulikua ukitumika kama eneo la mafunzo ya kitamaduni kwa jamii Yao, baada ya ongezeko la watu na ukataji wa miti na mapori msitu ulianza kupungua na wenyeji kuanza kupaelekeza kama Kisutu kidogo ikimaanisha msitu umebakia kidogo.

Kanga ya Kisutu ilitumika kama chaguzi mojawapo ya vazi la furaha la kumalizia mafunzo ya kitamaduni yaliyokua yakifanyika kwenye Msutu, kanga ya Kisutu iliashiria furaha na haikuwa ikivaliwa misibani au kwenye tukio la huzuni

Neno Kanga inayotambulisha vazi rasmi la jamii ya waswahili wa Tanzania ni neno linalopatikana Tanzania peke yake, vazi la kanga Linatambulika kwa majina tofauti na nchi za jirani za Tanzania

Aidha wakalimani hao wa Kiswahili wameiomba BAKITA kuanza mchakato ndani ya Tanzania wa kuikaribisha sikukuu ya Lugha ya Kiswahili Duniani Julai Saba kwa kuifanya Ijumaa ya kila wiki nchini Tanzania iwe siku ya kuvalia kanga ya Kisutu au vazi lolote linaloashiria asili ya Tanzania

Wakalimani hao pia wameomba watanzania kurejea utamaduni wa kuwapa watoto majina ya Kiswahili au ya asili za makabila yetu ya kitanzania, si vibaya watoto wakawa na majina mawili la kiasili na la Imani anayoamini, na upande wa Elimu wamependekeza kanga zianze kutumika kama mojawapo ya sare za shule, kwa wanafunzi kujifunga vilemba vya asili ya mswahili wa Tanzania

Mapendekezo hayo yalipokelewa na Ndugu Rajabu Kisawala kwa niaba ya Mama Consolata Mushi Katibu Mtendaji BAKITA na yako kwenye taratibu za kujadiliwa na BAKITA.

# Jenerali Sultani Makenga na historia ya umwagaji damu ndani ya DRC

UKILITAJA kundi la waasi la M23 linaloisumbua Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) kwa sasa toka kuanzishwa kwake na 'watu katili' waliowahi kupita hapo huwezi kulikosa jina la Jenerali Sultani Makenga.

Jenerali Makenga aliyehudumu kama Mkuu wa Jeshi la M23 na hata kuwahi kuwa kaimu rais wa kundi hilo pale alipomtimua Askofu Jean-Marie Runiga Lugerero, aliyekuwa akiliongoza hapo Februari 28, 2013.

Mbabe huyu Jenerali Sultani Makenga ni nani? Alianzia wapi? Kwa nini alipewa jukumu la kuongoza kikosi cha jeshi cha M23? Endelea…

Hapa ndipo unapoweza kujiuliza maswali mengi kuhusu kundi la M23, linafanya kazi kwa manufaa gani? Kwa nini lina nguvu kubwa na silaha za kisasa? Lengo lao ni lile la kuanzishwa kwake au ni 'batallion' ya kijeshi ya nchi fulani?Vipi Jumuiya ya Kimataifa inahaha kwa miaka mingi juu ya kundi hili na inashindwa kulimaliza? Maswali ni mengi kuliko majawabu. Unaweza kusaka jawabu na ukaishia kupata jibu tu.

M23 wakiwa wanaisumbua Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambayo ukubwa wake ni takriban sawa na Ulaya Magharibi, ni nchi kubwa katika eneo la Jangwa la Sahara.DR Congo imejaliwa kuwa na maliasili za kipekee, ikiwa pamoja na madini, uwezo wa uzalishaji umeme kwa maji, ardhi kubwa ya kilimo na yenye msitu wa pili kwa ukubwa duniani.

Hata hivyo kwa bahati mbaya, watu wengi nchini DRC hawajanufaika na utajiri huu.Historia ndefu ya uwepo kwa makundi ya waasi tofauti tofauti nchini humo kumesababisha migogoro, misukosuko ya kisiasa na ukosefu wa utulivu na kuwa chanzo cha matatizo mengi yanayowakabili raia.

> Mbabe huyu Jenerali Sultani Makenga ni nani? Alianzia wapi? Kwa nini alipewa jukumu la kuongoza kikosi cha jeshi cha M23?

Lakini ndani ya DRC, kuna makundi zaidi ya 100 ya waasi wenye silaha na yanajiendesha kwa kutumia rasilimali za taifa hilo.Jenerali Sultani Makenga aliyezaliwa Desemba 25, 1973 akiwa na miaka 50 kwa sasa, historia ya umwagaji damu ndani ya DRC haitamuacha salama hata kidogo.



Akizaliwa katika eneo la Rutshuru, Kivu Kaskazini, alifanikiwa kuongoza kikosi cha jeshi cha 'March 23 Movement' maarufu zaidi kama M23 aliwahi pia kuwa sehemu ya Rwandan Patriotic Front (RPF) wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Rwanda.

FARDC waliwahi kumpata?

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lishawahi kumjadili sana na hata viongozi wa juu wa M23 waliojaribu kumsogelea walijikuta wakipoteza nyadhifa zai. Inadaiwa Mei 2013 vikosi vya Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (FARDC) vilipambana na kundi hilo na kukaribia kumtia mkononi Jenerali Makenga.

Kuna hadithi ndefu juu ya shambulizi hilo, ila mashuhuda wanadai Makenga alijikuta katika majeraha makubwa kutokana na mapambano makali yaliyoendeshwa na pande hizo mbili.

Novemba 7, 2013, baada ya M23 kusambaratishwa na vikosi vya FARDC vikisaidiwa na vile vya Umoja wa Mataifa, vilimlazimisha Makenga akiwa na wapiganaji wake kujisalimisha wakiwa katika Hifadhi ya Taifa ya Mgahinga nchini Uganda.

Inadaiwa yeye na wapiganaji wake walihifadhiwa katika sehemu ya siri, ambayo haikujulikana.

Mwaka 2017, alirudi tena na kukusanya wapiganaji wake wapatao 200 na kuanzisha vita vya msituni ndani ya DRC, lakini jaribio lake lilishindwa huku wapiganaji wake wengi wakijisalimisha.



# Waamuzi wetu wana shida gani katika kutafsiri sheria?




Mwamuzi DANIEL BENNET wa Afrika Kusini aliwahi kuonyesha kadi nyekundu kwa mchezaji wa Esperance de Tunis AYMEN BEN AMOR iliyodhaniwa ilikuwa na utata, kwenye mchezo wa fainali ya pili ya CAF Champions League ambayo iliisha kwa matokeo ya 1-1 kwenye uwanja unaojulikana kama Stade 7 November pale Tunis.

Utata wa kadi ile uliisha baada ya picha za marejeo kumuonyesha Aymen Ben Amor akimtemea mate mchezaji wa TP Mazembe mara baada ya Harrison Afful kutoka Ghana kufunga bao la kuongoza la Esperance. Wakati anaokota mpira wavuni ili kuuwahisha katikati ya kiwanja kujaribu kutafuta mabao zaidi, njiani alimtemea mate mwenzie na refa Bennet aliona akakimbia naye mpaka katikati ya kiwanja, anauweka mpira chini tu akaonyeshwa kadi nyekundu.

Mchezaji akawa anajaribu kuuhadaa umma kwamba hakuna alichofanya, Camera za TV kwenye picha za marejeo zikamuonyesha akimtemea mate mchezaji wa TP Mazembe. Tukio hilikuonwa wakati wa purukushani ya kufunga bao, picha za marejeo ndo zikatupa ukweli.

Tangu juzi nahangaika kuangalia picha za tukio la Mokombozi wa Namungo kuonyeshwa kadi nyekundu ili nione kupitia TV nini hasa kilitokea lakini nimeshindwa kupata uhalisia, tunachokiona hakielezeki, hapa ndipo tunaposema pamoja na AzamTV kutuonyesha mechi zote LIVE lakini kuna maeneo hawatutendei haki. Hili tukio kama linavyosemwa kwamba Mkombozi alimkwida Ateba Korodani au alimpiga kibao, lingepaswa kuondolewa utata na picha za marejeo ya TV pekee kwakuwa VAR haijaanza kutumika.

Nimepata uhakika kutoka kwa maofisa wa ule mchezo wa jana kwamba mwamuzi Japhet Smart wa Katavi anasema Ateba alipigwa kibao na Mkombozi ndipo akamuonyesha Red Card! Swali ni kwanini hakutoa penati? Manake inaonekana kama tukio lilikuwa ndani ya eneo la 18 ya Namungo! Kuna shida mahali kwenye kutafsiri sheria.

Pamoja na shida ya Red Card, mwamuzi alipatia kwenye penati zote 3 alizotoa, kwangu hakuwa mwamuzi aliyemudu vyema mchezo, ameutimbangila ushindi wa Mnyama bila sababu za msingi, ameiteka show yeye ndio anatrend kuliko Jean Charles Anhou aliyeweka bao 2.

**BIN KAZUMARI MTIPA (The voice of the voiceless)**

FIKRAPEVU MICHEZO
JUMANNE, MACHI4 2025




# Arajiga, Kayoko waanza mafunzo ya VAR



Na Mwandishi Wetu


WAAMUZI 20 wakiwamo maarufu kama Ahmed Arajiga, Herry Sasii, Ramadhani Kayoko na Tatu Malogo, wameanza mafunzo maalum ya teknolojia ya usaidizi kwa waamuzi (VAR).

Kozi hiyo yenye lengo la kuboresha ufanisi wa waamuzi hao inafanyika kwa muda wa siku tano katika ukumbi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kuanzia leo Jumatatu hadi Ijumaa ya wiki hii chini ya mkufunzi wa VAR kutoka FIFA, Tameer Dorry.

Kwa mujibu wa orodha iliyotolewa na TFF, washiriki katika kozi hiyo ni Ahmed Aragija, Amina Kyando, Herry Sasii, Tatu Malogo, Nasir Siyah, Mohamed Simba, Ramadhan Kayoko, Alex Pangars, Abdallah Mwinyimkuu, Esther Adabert, Frank Komba, Kassim Seif na Ally Ramadhan.

Wengine ni Hamdani Said, Mohamed Mkono, Janeth Balama, Glory Tesha, Zawadi Yussuph, Siraji Mkwaju na Shaban Mussa.

## Aziz KI akabidhiwa 'Kariakoo Derby'




NA MWANDISHI WETU

MASHABIKI wa Yanga kama ilivyo kwa wenzao wa Simba wanachotamani ni kuona timu yao inashinda tu dhidi ya Simba na siyo vingine, lakini kazi hiyo licha ya kufanywa na wachezaji mbalimbali ndani ya kikosi cha Wananchi hao, lakini macho mengi zaidi yameelekezwa kwa 'Bwana harusi' Aziz Ki.

Staa huyo ndani ya kikosi cha Yanga hivi karibuni alidumu midomoni mwa mashabiki na wapenda burudani kwa ujumla, pale alipofunga ndoa ya kifahari na msanii maarufu Tanzania Hamisa Mobeto.

Muda mfupi baada ya kufanyika tukio hilo lililokusanya idadi kubwa ya mastaa Jijini Dar, mashabiki wa timu hiyo na hata wapinzani wao walianzisha minong'ono wakidai huenda kiwango cha mwamba huyo uwanjani kinaweza kupungua kutokana na matumizi ya ndoa yaliyomkabili kwa zaidi ya wiki nzima.

Lakini tofauti na matazamio hayo mwamba huyo akawa ndiyo kama amezidisha moto, kwani alikuwa akipachika mabao na kutoa asisti katika mechi mbalimbali zilizofuata na kuisaidia timu yeke kudumu kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu ikifikisha Pointi 58.

Uimara huo ndiyo uliomfanya awe tegemeo la kikosi hicho katika mechi hiyo muhimu ijayo Jumamosi hii itakayowakutanisha dhidi ya Simba, ambapo furaha ya mashabiki wa Wanajangwano hao ni kumuona Aziz Ki akianza kukitumikia kikosi cha kwanza.

Mechi hiyo imeanza kuteka simulizi kwa asilimia kubwa katika miji mbalimbali na hasa vijiwe vya mijini vinavyokutanisha mashabiki wa Simba na Yanga.

